## MATUMIZI YA FEDHA KANISA

**Wiki la kumi nane** Matumizi ya Fedha Kanisani ni kama ifuatavyo : 1. Wachungaji 2. Wamishonari na 3. Wajane tu wakati inahitajika (km Mjane wa wale walio kwenye Huduma) Ikiwa watu Kanisani mwako wako na nidhamu wataunga mkono huduma . Kanisa ambalo halijalipa bili zake ni aibu kwa jina la Yesu na inapaswa kuomba msamaha kwa wadeni wake, mara moja kurekebisha dosari, na kuzingatia mabadiliko uongozini (1 Tim. 3 Viongozi lazima wawe na sifa nzuri katika jamii) na "kwanza wadhibitishwe." Soma 2 Wafalme 4: 7 Mithali 3: 9-10, 27-29, 1 Wakorintho 9: 1-27, 1 Timotheo 5 ("Heshima" = Msaada) Wachungaji wanaungwa mkono na wahuduma wengine kifedha "kulisha kondoo" (Yohana 21), Hiyo ni, kuhakikisha kwamba kila Mkristo anafikia ukomavu hitajika, Wakolosai 1:28 (kukariri aya hii).

## NDUGU ATENDAYE DHAMBI

**Wiki la kumi tisa** na dhambi ni jukumu la kweli kwa viongozi Kanisani. Ikiwa hawashughulikii dhambi, basi viongozi wenyewe wanafanya dhambi. Andika nje hatua za kuchukuliwa na viongozi. Kumbuka 1 wakorinzo. 5 ambapo utaharibu Kanisa lako ikiwa utapuuza haya. Mathayo 18, 1 Wakorintho 4: 14-5: 13, 1 Timotheo 5: 19-25, Filemoni (kumrejesha ndugu).

## VYEO AMBAVYO UNAFAA KUJUA KWA AGANO JIPYA.

Waefeso 4:11 -17 (SOMA sura)

**Mitume** - Wanaume ambao Yesu mwenyewe aliwafundisha na kuwapa cheo hiki na nguvu ya miujiza Mathayo 10: 1-10. Matendo haya ya miujiza yalikuwa "ishara za Mitume" inasema 2 Wakorintho 12:12.

**Manabii** - Manabii wa Agano la Kale na labda katika Matendo. Kumbuka kuwa Waefeso 2: 20 inasoma kama "Mitume ambao pia ni manabii." Yesu na Mitume ambao pia ni Manabii, ndio msingi uliojengwa juu yake. " Wainjilisti na Mchungaji-Walimu huhubiri KWENYE MSINGI HUU.

**Wainjilisti** - Wanaume wanaotangaza habari njema ya Yesu Kristo.

**Wachungaji ambao ni Waalimu** (huu ndio msemo halisi wa Uigiriki) - Mchungaji ni neno linalo maanisha mtu anayelisha Kondoo. Wanalisha kwa Kufundisha.Maneno kadhaa yataelezea ofisi: A. 1 Timotheo 3: 1 - 2 "ofisi ya Askofu" au kiukweli "Episcopos" inamaanisha Mwangalizi au Msimamizi kwenye tovuti ya kazi. B. Tito 1: 5-9 Maaskofu Ni Wazee ("presbuteros**" C.** Wazee) Wale ambao sio wajanaga katika Imani! . Matendo 20:17 Wazee ni Wachunguzi (v. 20) na Ni Wachungaji . Hakuna Viongozi wengine juu ya Kanisa la mtaani. Ni tu: 1.WAZEE WA KANISA ( KI UMRI NA KIHEKIMA). 2. WAANGALIZI (ANAYE WEKA JICHO AU NYAPARA " "Episcopos" ). 3. WAJUNGAJI AU WAFUGAJI( ni yule anayeangalia, kuelekeza, kulinda na kulisha kondoo.) Kumbuka hiki ni kikundi cha vyiongozi kanisani wala si mtu mmoja. Mtu kati yao anayepata mafunzo maalum ni "Mchungaji ambaye pia ni Mwalimu." Anahudumu na Viongozi wengine . Mwalimu-Mwanafunzi.

2016 by Dennis Dickinson
whitestonemissions.com

# PROGRAMU KAMILI YA MAFUNZO YA BIBILIA

## SEHEMU YA TATU

## MAFUNZO YA VIONGOZI KANISANI.

1 Timotheo 3: 16-17 inasema kwamba maandiko ni pumzi ya Mungu, yatamzawadia mtu kwa kila kazi nzuri watakayomfanyia Bwana. Kwenye Yohana 8 Yesu alisema atamwachilia mtu kutoka utumwa wa dhambi kupitia Neno Lake (mafundisho). Utafiti huu utafuata muundo wa Bibilia kufunza maswala ya Uongozi. Kumbuka kuwa kwa Mungu tabia yako ndiyo kila kitu! Tabia mbaya badala ya kumcha Mungu ni wazi katika Yakobo 3-4 Mtu mwenye busara hujulikana "kwa tabia yake nzuri."

**Utangulizi 1**. Viongozi wa kanisa huchaguliwa kila wakati kwa sababu ya tabia zao nzuri na uaminifu kwa Mola wao. 1 Timotheo 3, Tito 1. Wanachaguliwa kila wakati na Viongozi wengine (sio wao wenyewe!). **2.** Viongozi wa Kanisa lazima waongoze! Kutokufanya chochote inamaanisha muhumini haongozi na anapaswa kujiuzulu nafasi yoyote aliyoshikilia ili kuwaruhusu wengine waongoze. wakati wa kusoma, Wanafunzi walikwenda na Yesu, wakisikiliza tu mwanzoni, wakitumikia, kisha wakawafikia na mwishowe wakawaongoza wengine. **3**. Viongozi wa Kanisa wanahitaji kujua Msingi wa Bibilia kwanza. Yesu hakufundisha Wanafunzi Msingi wa Bibilia! Tayari walikuwa na hilo kabla ya kuwa wanafunzi wa Yesu. Utafiti huu unatia muhuri ilivyokuwa,na Bibilia. Kiongozi wa Kanisa anapaswa kusoma Bibilia yote mwanzo. Baada ya hayo, maonyesho ya Vitabu vifuatavyo yatamfundisha Kiongozi wa Kanisa kwa kusoma sehemu na kupitia kila siku angalau wiki mbili. **Hii inafanywa WAKATI WANATUMIKA!** Mwongozo huu wa Funzo utashughulikia Vitabu vya Maandiko ambavyo vinaelezea Uteuzi wa Viongozi wa Kanisa. Hakuna mtu kuchichagua wala Kujipanga mwenyewe, na hata Mitume wenyewe hawaachiliwi kuondolewa, inasema Wagalatia 1 - Kumbuka Yuda!).

**VIONGOZI WAFUNZWE KWA KUFANYA!**

Viongozi walio Mafunzoni wanapaswa kuwa na Viongozi ambao wako tayari kwenye huduma. Kuangalia na kusaidia mwanzoni kama Wanafunzi. Wanapaswa kuwa katika Mikutano ya kamati ya Kanisa na Kuingiliana; ingawa bila mamlaka. Kwa miezi miwili majina yao yanapaswa kutumwa, au kutambuliwa kwa Kanisa, kwamba wanachukuliwa kuwa viongozi wa Kanisa. Hii inaruhusu watu kuelezea wasiwasi wowote juu ya tabia zao. Mwisho wa muda wa miezi miwili nikuthibitishwa tu. Hakuna mtu aliyekuwa Kiongozi wa Kanisa katika Bibilia kwa kupiga kura. "Wacha wathibitishwe kwanza" 1 Timotheo 3.

**SEHEMU YA TATU MAFUNZO YA UONGOZI**

Soma kila sehemu kila siku kwa angalau wiki moja. Zingatia Viongozi, Uteuzi wa Viongozi, utaratibu wa Kanisa na Walichofanya na kile hawakufanya.

# 1 **Injili ya Yohana;** Injili ya Wakristo. Anajibu Nani, Nini, Lini, Wapi, kwa nini na Jinsi gani anapaswa kudhibitishwa na kila mwamini. Inaelezea yale maandiko yanafanya, ya maandiko yanafanya wajibu wa Yesu, Roh na wahumini mtawalia. Maagizo kuhusu majukumu mbalmbali.

| | |
|---|---|
| **Wiki la kwanza** | **Yohana 1-6** |
| **Wiki la pili** | **Yohana 7-12** |
| **Wiki la tatu** | **Yohana 13-21** |

Matendo yanaelezea mwanzo wa Ukristo na mabadiliko kutoka Yerusalemu ya Uyahudi hadi mwisho ya dunia, au Kanisa la Mataifa.

| | |
|---|---|
| **Wiki la nne** | **Matendo 1-6** |
| **Wiki la tano** | **Matendo 7-11** |
| **Wiki la sita** | **Matendo 12-16** |
| **Wiki la saba** | **Matendo 17-22** |
| **Wiki la nane** | **Matendo 23-28** |

1 Timotheo Anaelezea muundo wa Kanisa la Mtaa. Fafanua kila neno kwa sura ya 3. **Wiki la tisa 1** Timotheo

2 Timotheo Anaelezea Ufuasi kwa Kanisa la mtaani. Ni nani ? Vipi?

**Wiki la kumi** 10 2 Timotheo

Tito Kupanda Kanisa la Mtaa. Vipi? **Wiki la kumi na moja** Tito 1, 2 Wakorintho Kurekebisha Kanisa la Mtaa lilovunjika = hekima YA KRISTO!

**Wiki la kumi na mbili 1 Wakorintho 1-9**

**Wiki la kumi na tatu 1 Wakorintho 10-16**

**Wiki la kumi na nne 2 Wakorintho 1-13**

Wagalatia Kurejesha Injili kwa Kanisa la Kmtaani.

**Wiki la kumi na tano Wagalatia**

Jinsi ya Kuwawashughulikia Wakristo wapya **Wiki la kumi na sita** 1,2 Wathesalonike, Filemoni (Maombi)

**Wiki la kumi na saba**: mpangilio wa kanisa la mtaani. Yakobo.